



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS –TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA
HALMASHAURI YA MJI NJOMBE



Unapojibu tafadhali taja:
KUMB.NA.NTC/E:P/152/522/1B/47

28/11/2023

TANGAZO LA NAFASI ZA KAZI ZA KUJITOLEA:

Mkurugenzi wa Halmashauri ya Mji Njombe anapenda kuwatangazia wananchi wote raia wa Tanzania wenye sifa, kuomba nafasi za kazi za kujitolea kama zifuatazo:-

AFISA MUUGUZI MSAIDIZI II (NAFASI 10)

Sifa zinazohitajika

Kuajiriwa wenye Stashahada (Diploma) ya Uuguzi, kutoka Chuo kinachotambuliwa na Serikali, waliosajiliwa na Baraza la Wauguzi na Wakunga Tanzania.

MAJUKUMU

- (i) Kutoa huduma za uuguzi;
- (ii) Kukusanya takwimu muhimu za afya;
- (iii) Kuwaelekeza kazi wauguzi walio chini yake;
- (iv) Kuelimisha wagonjwa na jamii kuhusu matatizo yao ya kiafya;
- (v) Kutoa huduma za kinga na uzazi;
- (vi) Kufanya kazi nyingine atakazopangiwa na mkuu wake wa kazi zinazohusiana na elimu, uzoefu na ujuzi wake.

MALIPO:

Mtumishi atalipwa posho kwa kuzingatia Uwezo wa Makusanyo ya kituo husika atakachopangiwa.

MUUGUZI II (Nafasi 30)

Sifa za Mwombaji:

Kuajiriwa wenye cheti cha Uuguzi cha miaka miwili kutoka katika Chuo kinachotambuliwana Serikali na kuandikishwa (Enrolled) na Baraza la Wauguzi na Wakunga Tanzania.

MAJUKUMU:

- (i) Kufanya kazi za kiuguzi za kuhudumia wateja katika jamii, hospitali na sehemu zote zinapotolewa huduma za afya.
- (ii) Kusimamia na kuratibu kazi zote za wahudumu wa afya katika Sehemu yake ya kazi
- (iii) Kukusanya takwimu na kutayarisha taarifa za utendaji wake wa kazi

- (iv) Kutoa huduma kwa wagonjwa majumbani.
- (v) Kutoa ushauri nasaha
- (vi) Kutoa huduma za kinga na uzazi wa mpango
- (vii) Kutoa huduma za uzazi na afya ya mtoto
- (viii) Kuelimisha wagonjwa na jamii kuhusu matatizo yao ya kiafya
- (ix) Kufuatilia utunzaji wa vitendea kazi katika maeneo yake ya kazi
- (x) Kufanya kazi nyingine atakazopangiwa na mkuu wake wa kazi zinazohusiana na elimu, uzoefu na ujuzi wake

MALIPO:

Mtumishi atalipwa posho kwa kuzingatia Uwezo wa Makusanyo ya kituo husika atakachopangiwa.

MTEKNOLOJIA MSAIDIZI MAABARA (Nafasi 5)

Sifa za Mwombaji

Kuajiriwa wenye cheti katika fani ya maabara kutoka Chuo kinachotambuliwa na Serikali na ambao wamesajiliwa na Mabaraza yao pale inapohusika

MAJUKUMU

- (i) Kuandaa vitendanishi (reagents) vya kufanyia vipimo vya Maabara.
- (ii) Kufanya kazi za awali sampuli zinazoletwa maabara
- (iii) Kukusanya damu kutoka kwa wagonjwa na watu wanaojitolea
- (iv) Kurekodi matokeo ya vipimo kwenye regista
- (v) Kutayarisha vifaa vya kazi.
- (vi) Kuhifadhi kwa mujibu wa taratibu sampuli zote zinazohitaji kuhifadhiwa baada ya uchunguzi.
- (vii) Kufanya kazi nyingine atakazopangiwa na mkuu wake wa kazi zinazohusiana na elimu, uzoefu na ujuzi wake.

MALIPO:

Mtumishi atalipwa posho kwa kuzingatia Uwezo wa Makusanyo ya kituo husika atakachopangiwa.

MTEKNOLOJIA MAABARA (Nafasi 5)

Kuajiriwa wenye Stashahada katika fani ya Maabara kutoka Chuo kinachotambuliwa na Serikali na ambao wamesajiliwa na Mabaraza pale inapohusika.

MAJUKUMU:

- (i) Kutunza vifaa vya maabara.
- (ii) Kufanya kazi za upimaji wa sampuli zinazoletwa maabara
- (iii) Kuhifadhi kumbukumbu za vipimo
- (iv) Kuwasilisha ripoti mbalimbali za vipimo katika mamlaka husika.
- (v) Kuagiza vifaa na vitendanishi vya kazi za maabara katika eneo lake la kazi
- (vi) Kufanya kazi nyingine atakazopangiwa na mkuu wake wa kazi zinazohusiana na elimu, uzoefu na ujuzi wake kulingana na ujuzi na uzoefu alionao.

MALIPO:

Mtumishi atalipwa posho kwa kuzingatia Uwezo wa Makusanyo ya kituo husika atakachopangiwa.

MASHARTI YA JUMLA KWA WAOMBAJI

1. Mwombaji awe raia wa Tanzania na mwenye umri wa miaka 18 na usiozidi miaka 45.
2. Mwombaji aambatishe nakala ya cheti cha kuzaliwa.
3. Mwombaji aambatishe maelezo binafsi yanayojitosheleza (Detailed C.V) yenye anuani na namba za simu za kuaminika pamoja na majina ya wadhamini (referees) watatu wa kuaminika.
4. Maombi yote yaambatane na nakala za vyeti vya taaluma, cheti cha kidato cha nne na cheti cha kuhitimu mafunzo husika.
5. Mwombaji aambatishe picha moja ya passport size ya hivi karibuni.
6. 'Testimonials, Provisional Results, Statement of Results HAVITAKUBALIWA.

Mwisho wa kutuma maombi ya kazi ni tarehe 08/12/2023 Siku ya Ijumaa saa 9:30 Alasiri.


Maombi yote yatumwe kwa njia ya barua pepe au anuani ya Posta kama ifuatavyo.


Mkurugenzi,
Halmashauri ya Mji
S.L.P 577,
NJOMBE

Anuani ya barua pepe:

utumishi@njombetc.go.tz

Imetolewa na:


K. A. Sadick
MKURUGENZI
HALMASHAURI YA MJI
NJOMBE.



NB :Tangazo hili linafuta tangazo la tarehe 24/11/2023